

YOUR

GUIDE

TO

UNIVERSITY

LIFE

U...

You can have fun and pass at the same time

Eunice Tossy Jonassy

To Helena, who believes we should all be real  
about life as a university student.

To those who are looking to the university life  
ahead of them with fear and anticipation.

# Contents

Introduction

Friendship and Relationships

Supplementary, Carry and Disco

Social Life

Faith and University Life

Migomo

Faking Life

Money Issues

Making The Most of Your Life in University- Grabbing opportunities and using resources to the maxi

Mean Teachers

Your Image

Your Health

Social Media

Affairs with Teachers (Sugar Teachers)

Things I learnt in my university life

## Introduction

Hello, hongera kwa kufika chuo. Kama kuna neno moja ningeambiwa nilitumie kuzungumzia maisha yangu ya chuo, ningesema "fun", because I had so much fun in university, so much time, money (which I thought was free), friends nearby and a lot of adventure. Lakini pia I made many mistakes, lost many friends, and had four supplementary in the course of four years that I was in the university. I wrote this book because I wanted people to know the reality early on, tunapokuwa vidato mara nyingi tunakuwa na ndoto moja tu... kufika chuo. Je, ukishafika chuo what's next? Tunapanga tu kuwa tutakula bata tukiwa chuo, na ndio sababu watu wengi wanashindwa kunavigate namna ya kutumia uhuru unaopatikana chuo na kujikuta wanafanya maamuzi mabaya mengi wakiwa chuo, this book will help you to avoid that and succeed in your university years. Najua chuo watakuwa wamekupa prospectus kuhusu chuo chao na a lot of instructions, ila hawajakupa guide ya jinsi ya kuface different situations zinazotokea ukiwa chuo, ili usiwe surprised and terrified as I was in my university years, be my guest.

## Friendship and Relationships

Woo-Hoo, hii ndio topic tunayoipenda vijana. Well toka ilipokuwa inaitwa reproduction halafu ikabadilishwa jina ikaitwa mahusiano, bado tupo nayo, sijui huko mbeleni itaitwaje ila tutaipenda tu.

### Friendship

Wanasemaga chuoni ndio sehemu unayoweza kupata marafiki wa maisha kwasababu utakuwa umekaa nao kwa muda mrefu ila pia ukiwa mtu mzima kwa hiyo unaelewa mpana wa marafiki wa aina gani unawataka (well sina uhakika na hili kwasababu bado naendelea kuishi kwenye maisha). Lakini pia wanasema chuoni ndio sehemu peke ambayo utakuwa unazungukwa na marafiki zako kwa ukaribu kuliko kipindi chochote, (hii ni kweli).

Unawaza kwamba utawapata wapi? Acha woga... Utakao kuwa nao course moja, utakutana nao canteen, utakao kaa nao room moja, sehemu za kidini, utakaofanya nao registration, chuo kizima kimejaa watu ambao ukiamua watakuwa marafiki zako, just choose wisely.

### How to make friends...

It's easy, make them. Oh no sio kirahisi namna hiyo. Kama umeenda bila friends from your previous education institution, you will feel lonely kwa muda, so feel it. It won't last long anyway, you will miss home pia, miss home as well. Kwasababu umeondoka home, lazima umiss, and tell you the truth, now that umeondoka home usidhanie kwamba kuna kipindi your life will be the same kama zamani ulivyokuwa unakaa home, because next

thing you know umepangiwa kazi mkoa/ nchi nyingine, so just miss home as much as you can.

Back to making friends, here are the tips:

-Be proactive, start talking to people. Usiogope anakuonaje kwasababu na yeye anawaza unamuonaje, so break the ice, start the friendship.

-Research the people that you want to be friends with and pursue them, nasema research kwasababu hao watu watakuja kukuimpact maisha yako negatively au positively kwahivyo inabidi uwe makini sana nao, if you can research them kabla ya kuwaingiza kwenye maisha yako, it will be good. (Use social media, or people close to them, ila isijulikane na usinitaje... ok bye).


-Share things, wanahitaji pencil wapatie.

-Be interested in their lives, wasikilize. People love to be heard so be a listener, utapata marafiki wengi (that's how I have friends mpaka leo, you are welcome).

-Please don't add them on Facebook, bila kuongea nao live kwanza, it is kind of creepy unless you are famous then they will feel privileged. Kutakuwa na swali kwamba sasa tukikutana are we friends or just in Facebook, tuavoid this tumia Facebook kuwa karibu na watu unaowafahamu, ndio sababu Facebook ilianzishwa.

But be careful of the people utakaowaweka kwenye maisha yako, wanawakilisha unavyoonekana kwenye jamii, so have fun "choosing" people. Tofauti na ndugu, ambao huwezi chagua, friends you can, so make sure you don't regret.

## How to keep friends in university?



Ili kuepuka lawama za ndugu na marafiki watakaosema kwamba unaringa kisa umefika chuo na ndio maana hauwatafuti, inabidi ujue kubalance kukeep mahusiano yako na watu wengine na urafiki ulio nao. And I got you, usiwaze.

Here is how you keep your people close:

-Make sure you call them, tumia muda unaoenda kununua chakula, kuchat au kuongea nao.

-Kumbuka matukio yao muhimu and be updated and post them on their birthdays or other events. (Unaweza set their birthdays on google calendar na kuwawish mapema, watahisi bado unawajali kwani umekumbuka bila kukumbushwa).

-Kwa marafiki zako walio off-campus, watembelee in between meals, have lunch with them or fanya

sleepovers. Sleepovers are always fun (but make sure huyo unayeenda kwake kulala anapenda pia).

-Spend weekends pamoja, kutoka out and etc

-If you miss someone specific siku hiyo mtafute, chances are they miss you too. Usipotezee kwasababu chances are anaweza akawa anapitia matatizo pia, you could be of help.

-Ukipigiwa kusaidia ishuru Fulani, saidia (ukipotezea tu, utaambiwa umebadilika toka ufike chuo haha). But kama hauwezi tumia hekima, usijisikie vibaya you can't solve everything all the time.

-Tengenezeni group la room, this way mtakuwa karibu wakati mnaishi pamoja.

-Watembelee ndugu zako walio karibu na mji/mkoa au nchi uliyopo (watakusaidia kwenye graduation haha). Lakini pia itakuwa chance yako ya kuwajua kwa undani.

-Set time, it's true kwamba hausomi masaa 24, so set time ya kusocialize, acha kuringa kisa umefika chuo!

## Relationships

Let me be open, majority ya wanaoenda chuo wanafikiri finally wanaweza kudate, kwasababu tumezuiliwa sana huku nyuma, tunajua kwamba chuo kuna freedom, so hata kudate utakuwa free. It is true, very true. Na ndio maana kuna couple nyingi sana chuo, na who is dating who ndio topic inayotrend mazingira ya chuo.

Here are the things I learnt kuhusu mahusiano ya chuo:

- 1) Sio siri, sijui watu wanajuaje but mkishaonekana mara mbili pamoja they know, na hata kama hamjawahi onekana wote, I don't know how people know aisee.
- 2) If you break up wakati mpo mazingira hayohayo, it gets weird and hard.
- 3) It is complicated kama mpo darasa moja.
- 4) They never last, some do, most don't.
- 5) They are peer pressure oriented, because ni topic kubwa sana ukiwa chuo and everywhere you go, you see people holding hands, it is easy kuanza mahusiano kwasababu ya hii pressure na sio love.

Mimi kama watu wengine I got my heart broken miezi ya mwanzo kabisa ya kufika chuo mpaka nikawa najiliwaza na "*Gavin DeGraw-am not over you*" kwasababu niliingia chuo na mentality ya kwa kuwa niko huru I can finally find mtu ambaye tutaoana and the first guy friend, was the one I decided was "the one". Got my heart broken mpaka nilipolearn my lesson. From the already heartbroken to the not-yet heartbroken, **DON'T RUSH**. Sio lazima the first guy or the girl awe wako, sio lazima upate mtu chuo, watu wanakutana popote pale maishani, this is not your end. Just because everyone is dating, doesn't mean you also have to date, study instead, eat, travel instead. You can save yourself from a lot of drama, pain, emotional stress, mawazo, kufeli na hurtful memory if you just take your time and not rush.

But hey, if you think uliyempata is the one you want for life, knock yourself out boo. By the way it is always fun kuwa na picha za toka mko university mpaka now mmeoana in your album, so go on.

My advice: Fanya decision hizi kwa kuangalia future yako,  
don't rush, home hawatakuelewa ukifeli kisa mahusiano.

## Supplementary, Carry Na Disco.

### Supp

Bado nakumbuka the first time nimepata supplementary, ilikuwa first semester ya mwaka wa tatu, na niliandikiwa supp katika lile somo na fail katika overall results, remind you sijawahi pata supp mpaka mwaka wa tatu. So I was shocked, fail? what do they mean by fail? Does that mean ndo nimefail chuo? Ndo naenda home? How am I going to face my mom? Nilikuwa kwenye kitanda changu cha hostel, juu, niliangalia matokeo kwenye simu, nilijiffeel kama umeme umepita kutoka kichwani mpaka miguuni (see I remember every detail, how can I forget?). By that time nilijilaumu kwanini nimecheza though sio kweli, nilijilaumu, nikajiona sina akili, ila nilimpigia rafiki yangu mmoja ambaye ni mjuzi kidogo wa supp, nikamuuliza ukiapata sup inaandikwaje kwenye matokeo, akanielezea, nikamwambia inaandikwa na fail akasema ndio, inakuwa pass kama umepass yote ila ukiwa na supp wanaandika fail kwenye overall, ndipo nilipotulia. Ila nilijiffeel mjinga wiki nzima, sikuwa na moyo wa kusoma semester ya pili kwa nguvu kama niliyokuwa nayo semester one, sikuwa motivated. Niliingia darasani the next day ambayo ilikuwa jumatatu, weeks baada ya kuanza semester ya pili na nikawa bado nawaza kuhusu ile supp. Nimepata supp nne katika course yangu iliyochukua miaka minne, moja kila semester katika mwaka wa tatu na wanne, ila woga wa supp ulikuwa unaondoka semester ya pili kwasababu tayari unajua hata matokeo yakiwaje unarudi tu kwenye conference so haina haja ya kuwaza sana. I don't know what it is about supp, ambacho kinatutisha ila nahisi the fact kwamba

unarudi wakati wenzio wanamalizia likizo, the fact kwamba wazazi wanajua haukufanya vizuri ule mtihani inabidi ukaurudie, au the fact kwamba this time usipofanya vizuri unaweza ukalirudia tena somo (carry). I wish, how I wish ningeambiwa kwamba mimi sio mjinga kwasababu nimepata supp japo kuwa kwenye matokeo imeandikwa fail, how I wish. Maana nisingejisikia mshtuko ule uliokuwepo kwangu almost semester nzima ya pili. Maana nisingejiona less than, ila normal.

Here is the thing, kila mtu ana njia yake ya maisha, so kuwepo chuo na kutopata supp na kuwepo chuo na kupata supp ni njia mbalimbali, no one is less than, kuna factor mbalimbali ambazo zinafanya mtu apate supp, sometimes mean teachers, sometimes binti wa kike kumkataa mwalimu, sometimes ni kuwa hilo somo haupo vizuri tu (huwezi kuwa perfect masomo yote na ndio maana mengine unafaulu unashangaa how did you make it). So if you are in university and you get a supp, wewe sio mjinga, and if you are in university and you didn't get supp, wewe sio T.O.

### Carry

Huwa nahisi sina haki ya kuongelea vitu ambavyo mimi personally sijavipitia, ila I have had two friends ambao walikuwa na carry. Pia ku carry somo hakumaanishi wewe ni mjinga, kuna kupa nafasi ya wewe kusoma tena lile somo kwa undani, na kulimaster. One of my friends aliekuwa na carry alifanya vizuri carry yake mpaka mwalimu akamuita, and infact alisoma vizuri mpaka mwaka wa mwisho hakupata supp kabisa, wakati miaka yote alipata, so cheer up, you will be alright.

## Disco

I realize naongelea vitu vikubwa sana katika maisha ya chuo, kwasababu vinaweza kubadilisha maisha yako ukiwa chuoni, I have seen two close people disco kwenye maisha yangu ya chuo, one was a classmate, one a friend. By disco I mean kudiscontinue (kutoendelea na masomo, mpaka baada ya kipindi cha muda Fulani). Unaweza disco kwa kucheat na kukamatwa, vyo vyingine ukifeli supp, ukiwa chini ya GPA (Grade point Average) Fulani (chuo changu ilikuwa 2.0) na sababu mbalimbali. I don't want to scare you, because life is too short to be scared, but live in faith and justly. That's how utakuwa na confidence ya kuface whatever will come, and Mungu atakupigania, you will make it, unless otherwise Mungu akiruhusu, go through it, and grow while going through it. Ishi tu ukifuata sheria na kuwa mwaminifu kwenye mitihani ili usikose confidence za kumuomba Mungu.

My Advice: Be serious na masomo yako, focus. Kama kitu hujui waulize wenzio au kamuulize mwalimu. Weka jitihada kwenye masomo, wengi huacha kuweka jitihada wakifika chuo kwasababu wanaona ndio muda wa kupumzika, but your grade matter, so soma kwa nguvu pia.

Nilivyofanyaga mitihani yangu ya supp ya kwanza kabisa nilikuwa naogopa majibu yatakayokuja, kwahiyo kujipa confidence niliweka screensaver picha iliyoandikwa "Whatever will come, will come and we will meet it when it does". So in your university life, whatever will come, will come, and you will meet it when it does come. Don't you live in fear.

## Social Life

I am a lover of fun; I love having fun. Ila nafikiri kwenye maisha ni vizuri mtu akijua hobby yake, things mtu anaenjoy kufanya. Most people change wakifika university kwasababu ile idea ya freedom inawapumbaza lakini pia naamini not identifying your priorities can be another factor.

Let's talk about freedom-

Most people wanasema ukifika chuo unakuwa huru, kweli. Ratiba zote except za darasani unajipangia, on the contrary na ukiwa home ambapo unakuta familia inakudirect sana, chuo inaonekana ni kipindi cha uhuru na kujitegemea. So how can you balance this freedom/ or how can you maximize this freedom?

- I advise kujua what you love doing, or what you plan on doing for fun

Hii itakuondolea kufanya vitu you don't want ila pia hautokuwa easily pressured na your peers

- I advise setting your priorities straight

Kuna watu ambao wakianza tabia wanapotelea moja kwa moja, I had a friend ambaye alipofika chuo alienda club ila baadae akaniambia anaacha kwasababu anaona anapotea kimasomo. I also heard a story of a friend of a friend who started clubbing and at the end of the day akasema anaacha chuo because it's boring, bora night life for him. Setting your priorities straight, and remembering kuwa you are going to the parties at night ni kwasababu ya

freedom unayoipata ukiwa uko chuo, once you go back home kuna ratiba nyingine chini ya nyumba ya mtu, so usifeli masomo.

-Having friends who tell you the truth

Friends utakaojisurround nao have a big impact on how you will live your life I believe, I think you need all kind of friends, but especially the ones who will tell you the truth kwamba you messed up, or hapa you did right.

-If you have an addictive personality kama mimi, stay away from drugs and alcohol, in fact, for your health, please stay away from drugs and alcohol.

Let me give you a couple of fun ideas that you can have at university, and how you can balance them well. By the way you are a social being, you need social life, so:

-Organize room parties with your roommates

-Organize house parties with those staying in off campus

-Go to the movies with friends

-Have lunch at the cafeteria (don't take it for granted, those are the things I have missed doing with my friends)

-Travel together, to another region, whether for mission or chochote, I advise kushiriki na religious organizations at your university, they make travelling cheaper and memorable.

-Travel alone on weekends

-Visit the museums, national parks or any historical site or monuments in the region you are in.

-Go camping

-Climb the mountains with your friends

-Just go to town and eat

-Surprise your friends on their birthdays

I advise doing these on weekends, they are the freest days, so fun, because there is no stress.

I advise on having fun, kwasababu you need both, studying and having fun. Don't stress on studies ukasahau kumake memories in your life, ukimaliza chuo you will look back and remember all the fun stuffs you did, just like I do now.

## Faith and the university life

Nadhani watu wengi wanafuata mambo ya dini kwa urahisi wakiwa nyumbani kwasababu ya wazazi, with that being said, naamini watu wengi walioshika dini wameshika kwasababu ya wazazi wao, ila tutoe wale ambao wako serious wao wenyewe. Na ndio maana tukiwa mbali na wazazi, yani tukiwa chuoni ni rahisi kuto kwenda sehemu za dini, kwasababu wazazi hawatuoni. As much as natamani nikwambie kwamba uwe serious na Mungu wewe kama wewe ila sio kwasababu ya wazazi wako, mi naomba tu nikuambie umuhimu wa kuna na mahusiano mazuri na Mungu ukiwa chuo/ au kumuomba Mungu ukiwa chuo.

- 1) Masomo magumu na sometimes walimu wanafanya yao, ila Mungu anaweza, so kumuomba Mungu ni muhimu ukiwa chuo.
- 2) Mmekusanyika watu wa aina mbalimbali sehemu moja, kuna vyuo vinawatu hadi 3000, am not saying wote ni wabaya, ila we both know kwa watu wengi kama hao watu wabaya #wachawi hawakosekani, unahitaji kumuomba Mungu ili akulinde.
- 3) Remember I told you about being careful with choosing your friends??? Well ukimuomba Mungu akuongoze kwa watu sahihi katika maisha yako anaweza kukuletea watu watakao kufaa maisha yako ya chuo
- 4) Strong friendships na bond nyingi nzuri zinatokeaga kwa watu wanaosali pamoja, those are the people who understand you on another level, so it is easy kuwa na loyal community by having this people.

- 5) As I said on having adventures and travelling to other places, religious institutions provide you with cheaper options, like when I went to Lake Ngozi with my chapel, fun and cheap.
- 6) I believe ukiwa na watu mnaoamini kitu kimoja, they can keep you grounded, kama unashindwa kujicontrol in stuffs wanaweza kukusaidia, hata ukikosa ada, in our chapel tulikuwa tunachangiana in that way, that is community right there.

So it's amazing that in this guide to your university life, I advise you to know God more in university, hii ndio nafasi ya kumjua Mungu ukiwa peke yako, na kumuona kwenye maisha yako mbali ya kumuona kupitia wazazi, so go on this journey alone and with the community that you will find at your university. Ni kweli watu huwa wanamuacha Mungu/kuacha mambo ya Mungu wakifika chuo kwasababu ya freedom or social life kama nilivyoongelea kwenye chapter iliyopita, but you don't have to be one of them.

## Migomo

Imetokea vyyo vingi, na umeshasikia. But take it from me, mi naamini kuna watu wameitiwa kupigania haki, and they can even die for that, and pia naamini kuna wengine ni watazamaji tu in life. Kuna watu kama Mwalimu Nyerere na kuna babu yangu, two different people probably kwenye same era. I personally believe in open talks, open communication on a personal level kwenye kusolve vitu, but since migomo imeanza kutumika in some places na hapa pia tumeiadopt. In no way do I support migomo, and unless you are revolutionist who is ready to die and lose your education for a cause that you think won't be solved by talking, starting a change.org campaign, or by kukusanya hela from the community and bringing the change, well knock yourself out boo.

I believe we are change agents, and there are so many ways to bring change, but I from experience sidhani migomo hasa kwa watu wengi ni efficient.

When I was in the second year, kulikuwa na mwalimu aliyekuwa anasema maneno ya vitisho kwetu, and tukafanya mgomo ili abadilishwe, now yule mwalimu ni mwalimu wa department yetu, so tukaenda department, tukasign form ya kumuondoa na technically tukawa tumegoma kufundishwa naye, wakuu wa department walikaa vikao na sisi, mpaka mwisho but then hatukubadilishiwa mwalimu for several reasons. First of all, this was brave, so brave kwasababu walimu hawatakiwi kututishia maishani ila kutusaidia kufaulu. Sijui kwanini mwalimu anajisifia wanafunzi wanaofeli somo lake wanapokuwa wengi,

kwabababu wengi wanapofeli inaonesha kwamba mwalimu hajui kufundisha na ndio maana wengi wamefeli, but sijui wao kwa nini wanajisifia, and kututishia in anyway na sio kutusaidia na hiyo ni abuse of power.

So that was brave, but costful, kwabababu binadamu wanavinyongo lakini pia hakuna anayependa kuonekana mbaya, lakini pia mkishakuwa wengi kila mtu hufwata maslahi yake kwahiyo ni rahisi kugeukana na chuoni ni mahali ambapo mwalimu anaweza kukuchukia na kukushikia kinyongo miaka na miaka for just one thing you did, sisemi uishi kwa woga au unyanyasike, seek help. So from experience nashauri peace talks na sio migomo, mazungumzo naona yako more efficient.

## Faking life

Ni kweli kuna watu wanaishi maisha ya uongo, ambayo yanakuwa ya gharama kwao. To fake life is the most expensive and tiring thing for someone to do. And financial aids kama boom zinawezesha hii tabia kwa namna moja ama nyingine. Na kwa vile pia watu hawakujui ndio wamekuona ni rahisi sana kuwaigizia, but why watu wanaigiza in the first place????

Here is the reason: kwenye maisha kuna classes, in this capitalistic culture, kuna caste, kuna the rich, middle class na the poor. Pia kama binadamu una emotions, una pride na una pain in one way or another. Mazingira ya chuo yanakukutanisha na watu wa classes mbalimbali ambao wanaweza wakakufanya ujisikie wivu, wakakuintimadate, au wakakufanya utake kuigiza ili kucatch up (ili kuficha your reality au kuringana nao), na hii ni sana kwa wale wanaojaribu kuficha hali zao za kiuchumi za nyumbani. Na mimi sishauri ujitangaze (hello, I am rich, nice to meet you, nah) but pia sishauri kuingia cost ya kukeep na maisha ambayo kwasasa hauyahitaji au kwasasa hauna financial means ya kuyaishi, watu husema unaishi kutokana na kiwango cha fedha unachokipata, so you will afford that life but kwasasa tumia ilo boom kwa mambo ambayo nitakushirikisha kwenye chapter ya money issues.



Kuna aina nyingine ya kufake maisha, ya kuwa mtu ambaye wewe sio. I don't expect you to know yourself much right now, because I also figured myself better in

university. Ila kuna wale ambao hata ex-schoolmate wao wanasema yule amebadilika shule hakuwa vile. That's another issue. Don't try to fit in kwenye university vibe, au in a group of friends so bad kiasi kwamba unajibadilisha kabisa who you are, to the extent wewe pia haujui who you are anymore. That's fake, be real, be you, know you, speak you and live you.

## Money issues

### -Things I wish I knew about money in university

- 1) You can maximize it, kwa kuanzisha biashara (ya chakula, vocha or whatever). This is the time in your life where you are face to face with someone who can buy your product, start a business.
- 2) You can put them in a fixed account ili izalishe baada ya miezi Fulani.
- 3) You can save some amount kwaajili ya life after university, kama ukisave 50,000 kwa kila hela itakayoingia it means ukimaliza chuo unahela ya kukusaidia hata nauli wakati wa kwenda kuombea kazi.
- 4) There will come a time utaoilipa hela (boom) unayoitumia kwa fujo/ or kistaarabu, whatever utailipa.



Let's talk about money. The only thing I want to tell you is to learn how to manage your money early on, know how it can bring more and learn how to make it count when you use it.

How to manage money- you can download apps zinazorecord your spending, earning n.k. Or you can read books about money, whatever you do, make sure you learn how to manage money early on. How you manage your money right now, will have an impact on how you will for the rest of your life. I think wanafunzi wanatumia hela sana kwenye vocha because I also did, ila unaweza

ukatamia university Wi-Fi in some weeks, when it comes to food, unaweza ukaweka bill sehemu to save some money, don't buy things you didn't plan too, ukienda mahali nenda na the exact amount you will need, so that you won't be tempted etc.

How it can bring more- see things I wish I knew about money in university

How to make it count when you use it- well help people, fund some projects, peleka vitu kwa watoto yatima, toa sadaka, ukipata buy yourself something memorable or food so that you can remember what you did when you earned it (treat yourself) etc.

## Making The Most of Your Life in University- Grabbing opportunities and using resources to the maxi

Chuo kuna a lot of opportunities, a lot, a lot, a lot and grab as many as you can please.

- 1) Free Wi-Fi, use it as much as you can, there is no other place utapata free Wi-Fi for yourself, free kama chuo, kazini utatakiwa kuwafanyia kazi plus I think wanajua ukifanya vitu vyako.
- 2) Driving course or any other learning course (I took Chinese language classes in university, you can too and more).
- 3) Travelling opportunities
- 4) Get a passport or open accounts (it is easy kufanya vitu kama kufungua account au kupata passport ukiwa chuo kwasababu dean anakudhamini but ukitoka chuo process ni ndefu, so make the most out of your time).
- 5) Make friendship with teachers wawe your referees.
- 6) Learn different stuffs on YouTube, remember Wi-Fi is free.
- 7) Workshops zinazofanywa kwaajili ya wanafunzi then wanawapa cheti, grab them!!!!
- 8) Volunteering opportunities za aina zozote.
- 9) They want people to represent the university anywhere, go!!
- 10) Leadership opportunities, do them.
- 11) Join sports team, ujifunze michezo or ulete ushindi chuo ukiwa unakiwakilisha kwenye

mashindano. (My favorite being tennis, volley ball, and basketball).

12) Learn how to play instruments, either piano or guitar in chapels, learn anything new and useful for your life hata music engineering. I was a dj in university, I used virtual dj kupiga nyimbo in chapel, so in events za chapel I was a hit, the best in fact.

13) Read books, sio tu za masomo yako, ila za maisha kwa ujumla. Ukiwa chuo you have plenty of time kama haujiandai na mitihani, you can use this time kusoma vitabu or to do a million of other creative things that you can do, write poems, kuwa MC or whatever, just develop yourself. Katika ulimwengu wa sasa experience ya vitu vingi ni muhimu kuliko cheti chenye grades tu.

14) Start a YouTube channel or a blog, there is free Wi-Fi remember??

I went to China for the first time in my life when I was in university, because I grabbed opportunities when they came.

## Mean Teachers

As I shared kwenye migomo chapter, mi pia nimekutana na mean teachers, hapa naongelea wale walimu ambao wanafanya tu roho mbaya, hata kama umefaulu wanakuwa na roho mbaya na wanajulikana kwa roho mbaya yao. Of course the world is not full of kind people, it could have been boring if all of us were kind, no diversity and adversity. I hope and pray that you won't meet them but maybe you will, because they are there.

Mara nyingi I have always tried to understand how people are and why they do what they do, including evil, now when it comes to teachers being mean there are several reasons I have figured out:

-Sifa na umaarufu, ni rahisi sana hawa walimu wabaya kuwa wanajulikana kwasababu wanachukiwa, kwahiyo they don't care if you hate them, they just love the fact that you know them.

-Revenge, maybe na wao wamekutana na mean teachers before, they suffered, wanataka na wewe upitie magumu as well.

-Matatizo ya kisaikolojia, although revenge pia ni tatizo la kushindwa kusamehe, ila hapa naongelea upbringing yake, naongelea maumivu huyo mwalimu (kama binadamu) anayokuwa ameyabeba toka zamani, hapa naongelea matatizo kwenye familia yanayoharibu saikolojia yake na kumfanya awe na roho mbaya, you never know what someone is going through, same applies to mean teachers, we just never know what they are going through in life.

## How can you deal with them??

-Nenda kwenye vipindi vyao, most of the time wanakuwaga na IQ kubwa wanajua majina ya wanafunzi wote na sura zao. Ukienda kwenye kipindi haumpi nafasi ya kukutafutia sababu. (Plus this is the only advise I would give everyone, please go to class, kudodge ni sababu nyingine nilipata supp mbili).

-Stay away from talking behind their backs, most of the times wana wanafunzi ambao wameshaenda kujipendekeza kwao, kwahiyo hao huwa spies zao. By the way kwanini ugossip kuhusu mtu, mean or not, sio tabia nzuri.

-Be nice to them, you don't know what they are going through, so just be nice to everyone.

-Pia usijipendekeze, we had this one mean teacher he never cared umejipendekeza or not, alimpa supp hadi mtu aliyeenda kujipendekeza so I advise just live your life, just be responsible, just do what a good student does, stay out of trouble ili isikucost.

## Your Image

Here I want to talk about how you present yourself to people. Najua high school or whatever your education background is, haukujali kuhusu how people see you, well now you need to care. Because dunia hainaga watu wapya. Uliokutana nao shule utakutana nao kazini, uliokuwa nao primary umekutana nao chuoni, na uliosoma nao watafanya kazi na watu uliocheza nao, uliosoma nao primary watafanya kazi na uliosoma nao chuoni, yani dunia haina watu wapya. Image yako au vile unajipresent kwa watu itabaki, watasahau kila kitu ila hawatosahau kwamba wewe ni muongo, ulikuwa mhuni, ulikuwa hiki ulikuwa kile. Na unaweza kuta unataka kwenda kuomba kazi sehemu Fulani but huyu anamjua yule, na yule anajua ulikuwa mwizi chuo, so unakosa kazi. Be careful and present yourself well, care about your image, your honor. Again simaanishi uigize na maanisha ukue, uishi maisha as a responsible adult.

Kwa mfano kipindi mimi niko chuo, tulikuwa na hizo scandal na mnajua Fulani kafanya hivi na vile and everything else, au yule ukikaa nae room moja ana roho mbaya au mchafu and etc. tell you what hivyo ndio vitu watavitangaza ukimaliza chuo, you might think it is temporary na watu wachache ila dunia nzima itajua kwasababu mtu anaweza kutolea mfano hata miaka na miaka ijayo kuhusu jambo moja tu ulilofinya ambalo halikuwa na athari kwa wakati huo au wakati unalolifanya ulihisi ni kwaajili ya umaarufu or ni trend kulifanya.

## Your Health

Now that unajitegemea mwenyewe kwenye kula inaweza kuwa tempting kula unhealthy things, and not to take care of your health. I, for example nilikuwa nakula chipsi kila siku kuanzia mwaka wa kwanza mpaka watatu, mchana na jioni, nikibadilisha ni siku moja moja, kwasababu niliamini now that siko home am free kula chochote, which was true but sikutakiwa kuneglect afya yangu, the results niligain weight, na am still working out to be fit now but I wish I could have then.

Be serious about your health, ukianza kumwa how can you study? Your health is the only reason, you are still waking up in the morning and going to class, so take care of it, be serious about taking care of it.

Here is how you do that:

-Usipige pasi ndefu unless umefunga, hata kama umebanwa sana jitahidi basi uwe hata na mkate.

-Balance your meals, eat balanced diet, kula na matunda pia.

-Fanya mazoezi, hii inafaa pia hata kwaajili ya akili, mazoezi yana stimulate ubongo pia katika kufikiri. Ukitenga hata lisaa limoja kwaajili ya gym au hata kukimbia au kujoin basketball team or tennis, it is good for you.

-Drink a lot of water, stay hydrated please.

-Balance muda wako wakuangalia movies, it is not healthy macho yako kila saa kuwa kwenye screen

unaangalia movie, nilipoingia chuo nilikuwa naona vizuri hadi mbali, but baada ya mikesha ya movie and everything sasa sioni mbali, and sitaki kuvaa miwani na kwenda hospital, but I don't want you to be like me so please balance your screen time.

- Take care of your dental health, meno yako yasafishe, usile nyama sana and sugary stuffs. I tell you this because now I go to the hospital every Monday to see my dentist kwasababu nilikuwa nakula nyama every meal na meno yanasumbua inabidi nizibe.

-Pia usafi wako wa mwili, na kufua nguo, set time for those pia, take care of yourself and love yourself.

-Nenda hospital the minute that you think you are unwell, or panga muda wa kuwa unaenda kucheck afya, now that una kadi ya afya itumie ipasavyo.

Don't neglect yourself, neglecting your health is hating yourself.

## Social Media

We love to be up to date, social media is the tool inayotusaidia. We love to get attention and show off (how beautiful our lives are, or jinsi tulivyopendeza), social media is the tool inayotusaidia. But when it comes to your studies, you need to balance. I remember kwenye group discussions wakati tunafanya assignments na watu wako busy kwenye social media, hawachangii chochote, ila wanachat, ilikuwa inaboa ila pia ilikuwa inatupotezea muda sana.

Here is how you balance your social media use na masomo yako:

-Set time ya kuview social media, either asubuhi or jioni, or muda Fulani ambao unahisi utakufaa na stick to it, every day.

- Give yourself breaks, kama una mitihani haina haja sana ya kucheck social media kwasababu sio notes, chukua break kipindi chote cha mitihani.

-Check your social media usage, wengi hucheki wakiwa wameboreka, and if you are one of them then you are using social media as therapy, na utakuwa unaitumia zaidi ya unavyotakiwa, learn how you can control yourself.

-Get a hobby, mimi nimetoka kwenye social media zote nilipokuwa mwaka wa tatu kwasababu niliona natumia muda mwingi na bundle lingi, na nilimuuliza rafiki yangu ambaye hayuko social media, nikamuuliza what do you usually do now that you are not on social media, akaniambia "get a hobby". Tafuta kitu unachokipenda

kufanya fanya, wakati wewe uko facebook toka saa tisa mpaka saa kumi na mbili, kuna mtu anacheza basketball, or anajifunza kupiga piano or anything. So just get something else kinacho stimulate ubongo wako, kuliko gossips za social media.

-Don't check social media ukiwa class, in fact nashauri uache simu room ukiwa unaenda class, not only unaonesha heshima, ila pia itakusaidia kuelewa na kuwepo darasani 100%.

-Don't check social media ukiwa unadiscuss na wenzio.

-Don't check social media ukiwa unasoma, weka silent simu, weka mbali. Muda mwingi tunaupoteza kwa kuangalia social media halafu unakuta haujasoma kitu.

## Affairs with Teachers (Sugar Teachers)

Kabla sijaenda chuo nilisikia story za walimu wanaotaka wanafunzi na kuwafelisha, so kabla sijaenda nilifunga nakuomba Mungu aniepushie kukutana na walimu hao, God is good sikukutana na hilo, but imagine a world whereby someone has to pray for God's protection in an environment where the teachers are supposed to be our guardian parents when we are with them. And this is the world we live in, I have had friends and I have seen victims, and I have had stories, stories of a girl alieshikwa makalio canteen na mwalimu, and she could do nothing, she had to act like it did not happen, stories of a girl who slept with a teacher ili atolewe supplementary, stories of a girl aliefungiwa ofisini na mwalimu akitaka kumbaka but the good thing is kuna mtu aligonga mlango, but also stories of female students wanaotoka na walimu just for money, fame or advantages that come with going out with those teachers. And this is the world we live in. Kuna siku nilikuwa naongea na my roommates na tulikuwa tunatafuta namna ya kulisolve hili, and mmoja wetu akasema "where can we go? mtu unayeenda kumshtakia nayeye pia anafanya tabia hizo, na walimu wana ushirikiano kwa hiyo ukienda kwake atamuonya mwenzie, na akimuonya ujue haufaulu tena kwasababu atakufanyia roho mbaya kisa ulienda kumsema". There are few times in my life when I have felt powerless, one of those times ni siku hiyo, unajua mara nyingi tunaona hawa wadada as wao ndo wanatabia mbaya kwa kufanya haya mambo, na in no way natetea or napendekeza hii tabia. But if we could have walked in their shoes probably we would have done that and more. Yes, kuna watu huwa hawakubali kufanya hayo, na mimi si support watu

kutoka na walimu for their grades, nakumbuka jumapili moja kanisani pastor alitoa ushuhuda wa binti ambaye alidiscosishwa na mwalimu kwasababu alimkata, she was depressed akarudi home lakini Mungu akamfanyia muujiza akaenda kusoma Marekani, Yes God is faithful, na we have to live like the way she did, but my question is why in the first place? Why do women have to be put in a place ambayo their brains are not the one determining their academic achievements ila their bodies? This is something that is not openly talked about, but it exists in university life.

I believe God created men physically stronger not to harm, harass or abuse women, ila in the world we live in today that's what majority do. Kuna idara ya wanawake na viongozi wao kwa ishuhada kama hizi, but I hate the fact that idara kama hiyo inabidi iwepo in this world, why does it have to be so unsafe mpaka tupate idara kama hiyo? But still, please go see them if you are facing these things. In university women should be united, kwasababu wanaface vitu vilivyo sawa katika mazingira hayo, have the WhatsApp or Telegram group for all the women, to openly share these issues.

To students who are cornered and give in:

If you haven't yet, don't. Seek help, speak out, be brave. He might think maisha yako yapo mikononi mwake, but remember that maisha yake pia, infact maisha yenu wote wawili yapo mikononi mwa Mungu, He is the One more powerful than him.

Even if you have already, I advise walk out of it. It's not worth it.

There are other affairs ambazo they just happen because people think teachers have money, well graduate with A, not AIDS. Just think kabla yako walikuwepo wanafunzi wangapi? And more what do you gain by that kama sio temporary pleasure and AIDS? Don't mess up your life, graduate, you will earn your own money.

My Advice: Don't be judgmental, try to understand the story from the person, and be there for her, or him if it happens to a guy. You are making the world a better place by taking a stand, and by leaving that teacher you are making your building your own future.

## Things I learnt in my university life

- Kushirikiana na watu, na kushare vitu na watu.
- To be there for people.
- To have fun in whatever situation I am in.
- To know that it will work out at the end, see I am graduating, it worked out.
- To make the most out of my life
- To make friends, and how to leave the ones that I think are bad for me
- To have a stand, and my own standard
- That my opinion matter

## A author's Note

Hey, am so excited for all the memories that you will make in university, am so excited for the life you will live there, and the one after university. You are an adult now, take responsibility of your life and how you direct your future to be. Yes, you can have fun and pass at the same time, just like I did, and the others before us did. Thank you for reading this guide, I have tried to share my experience, successes and failures so that you can learn from both, I did this because I want you to have fun and pass in university, and I believe you can.

Keep me updated with what is going on in your university life at [euniefodie@gmail.com](mailto:euniefodie@gmail.com). I would love to hear and see how you are having fun and passing at the same time.

## About the Author

Eunice Tossy Jonassy ni graduate wa mwaka 2018, anayependa kula, kusafiri na ice-cream. Pia anapenda kwenda beach na kuandika. Anaandika kwenye blogu yake inayohusu maisha ya chuo inayoitwa [maishayachuo.blogspot.com](http://maishayachuo.blogspot.com)

Kwa ushauri, maswali, comment au chochote kuhusu maisha ya chuo, nitafute kwenye email, [euniefodie@gmail.com](mailto:euniefodie@gmail.com)

Au pia kwenye blog, [maishayachuo.blogspot.com](http://maishayachuo.blogspot.com)